BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA NA MASHIRIKA (LAAC) KUHUSU UWASILISHAJI WA RIPOTI ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI, KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa rehema na mwenye kurehemu kwa kutujaalia uzima na afya njema na kuweza kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa na wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) kuhusu uwasilishaji wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa Serikali za Mitaa, Mashirika, Taasisi za Serikali Zinazojitegemea na Ripoti ya Mifumo ya TEHAMA kwa Taasisi za SMZ kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyoelewa kuwa ni mara ya kwanza kwa Kamati ya LAAC kuwasilisha Hotuba ya Maoni yake ikiwa haina Mwenyekiti, hii ni kutokana na kufuatia kifo cha Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mnasaba huo, kwa niaba ya Kamati ya LAAC tunaomba kumuombea dua aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii Marehemu Mheshimiwa Habib Ali Mohammed na tunamuomba Mwenyezi Mungu amsamehe makosa yake, amjaalie kauli thabiti na pepo ya Firdous iwe ndio makaazi yake na sisi tuliobaki tunamuomba Mwenyezi Mungu atujalie mwisho mema AAMIIN.

Mheshimiwa Spika, pia, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa kuweza kuwasilisha Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi linalojadili bajeti kama ilivyozoweleka.

Mheshimiwa Spika, shukurani za pekee zimfikie Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya ya kufuatilia fedha za Umma na kutoa ushauri juu ya namna kufanya matumizi ya fedha hizo kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii kwa mashirikiano yao wanayonipatia wakati wote wa kazi za Kamati ikiwa ni pamoja na wakati wa kuzipitia, kuzichambua na kuzijadili taarifa hizi muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu azidi kutupa nguvu ili tuweze kutekeleza vyema majukumu tuliyopewa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwataja kwa majina Wajumbe na Makatibu wa Kamati ya LAAC kama ifuatavyo:

NAM.	JINA KAMILI	NAFASI
1.	Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	Makamo Mwenyekiti
2.	Mhe. Bakar Hamad Bakar	Mjumbe
3.	Mhe. Haji Shaaban Wazir	Mjumbe
4.	Mhe. Shadya Mohammed Suleiman	Mjumbe
5.	Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe
6.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	Katibu
7.	Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi	Katibu

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha Ripoti za Ukaguzi mbele ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kupokea ripoti hizo kutoka kwa Mheshimiwa Rais na kuzifanyia kazi ni wazi kuwa Afisi hizi mbili zinatekeleza majukumu yake vyema kama Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC katika kuzipitia Ripoti hizo, imebaini kuongezeka kwa makusanyo ya mapato kwa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea, hata hivyo, mifumo ya ukusanyaji mapato bado inakabiliwa na changamato kadhaa ambazo zinapelekea mianya ya upotevu wa mapato

hayo kama vile, kuwepo kwa mapato ambayo hayana makadirio ya makusanyo, ukusanyaji wa mapato bila ya kujulikana chanzo halisi cha mapato hayo na kuwepo kwa mapato yaliyokusanywa nje ya mfumo ambayo yameshindwa kuthibitishwa iwapo kama mapato hayo yaliingizwa yote Benki au vvenginevyo.

Mheshimwa Spika, kwa mfano Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) imekusanya jumla ya Tsh. 310,268,309 kupitia vyanzo vyake mbalimbali vya mapato na mapato hayo yameonekana kulipwa moja kwa moja benki pasi na kuzingatia (control number) zilizotolewa na Mamlaka, jambo ambalo linaashiria kuwepo kwa malipo nje ya mfumo kwa kutozingatia "control number" hali inayoashiria kuwepo kwa upotevu wa baadhi ya mapato ya Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inasisitiza kwa mara nyengine tena kwa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea juu ya muendelezo wa usimamizi mzuri wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato, uwazi katika kupanga makadirio ya mapato na ukusanyaji halisi wa mapato kwa kila chanzo husika kwa lengo la kuonesha uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji na kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato hayo

Mheshimiwa Spika, hadi leo hii bado kuna baadhi ya Mashirika na Taasisi Zinazojitegemea hazina usimamizi mzuri wa matumizi ya fedha za umma kwa kushidwa kuthibitisha uhalali wa baadhi ya matumizi hayo jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa Taasisi zilizoripotiwa kwenye Ripoti za Mdhibiti ni Wakala wa Uchapaji Zanzibar (ZAGPA) ambayo imefanya matumizi ya kifungu cha Honoraria chenye jumla ya Tsh. 55,463,034. Dosari iliyobainika katika matumizi hayo ni kukosekana kwa uhalali wa matumizi kutokana na kutojulikana kwa aliyelipwa, aliyeidhinisha malipo hayo pamoja na wanaohusika kulipwa kwa mujibu wa utaratibu.

Mheshimiwa Spika, Ripoti za Mdhibiti bado zinaendelea kubaini kutofuatwa kikamilifu kwa Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 pamoja na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kwa Mashirika na Taasisi Zinazojitegemea.

Mheshimiwa Spika, kwa kulithibitisha hilo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imefanya manunuzi ya Tsh. 632,524,845 bila ya kufuata kifungu nambari 68(2) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Mwaka 2016 kinachozungumzia juu ya uitishwaji wa zabuni ya wazi kwa

kiwango ambacho kimefikiwa katika Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Mheshimiwa Spika, Mifumo ya udhibiti wa ndani kwa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea imeimarika ukilinganisha na mwaka uliopita kwani kati ya Taasisi thelathini na tisa (39) zilizokaguliwa ni Taasisi tano (5) tu ndizo zilizokuwa na dosari katika Kamati za Ukaguzi wa ndani na mapungufu katika Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani (Internal Audit Unit).

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inazipongeza taasisi zote ambazo zimeweza kuimarisha mifumo yake ya ndani ya udhibiti ambayo kwa kiasi kikubwa ndiyo inayoleta chachu ya kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati ya LAAC inazitaka Taasisi hizo tano (5) kuufanyia kazi ushauri wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali haraka iwezekanavyo ili hoja hii isijitokeze tena katika kaguzi zijazo, miongoni mwa Taasisi hizo ni Shirikala la Meli na Uwakala Zanzibar, Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Pemba.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inaendelea kuyapongeza Mashirika, Taasisi Zinazojitegemea na Serikali za Mitaa kwa kuwasilisha taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka kwa wakati katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inatoa pongezi hizo kwa kuwa kuwasilishwa kwa taarifa hizo kunatoa nafasi kubwa kwa Serikali katika kupanga mipango yake mbali mbali kwa maendeleo ya nchi na wananchi wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwasilisha hesabu hizo kwa wakati lakini bado, Taasisi za Serikali haziandai taarifa ndogo za fedha ‘Segment Report’ kama zilivyoelekezwa na Afisi ya Rais, Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inazidi kulisisitiza suala hilo kwani endapo Taasisi zitafunga hesabu kwa kutumia mfumo huo itaiwezesha Serikali kupima utendaji wa Taasisi fulani katika eneo husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inaunga mkono ushauri ulitolewa na Mdhibiti kwa kuitaka Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kutoa mafunzo endelevu kwa Taasisi za Serikali kuhusiana na kuandaa taarifa ndogo za fedha ili ziweze kuendana na mabadiliko yanayotarajiwa kujitokeza ya kuhama katika mfumo wa “Cash basis” kwenda “Accrual Basis”.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ukaguzi wa Serikali za Mitaa Kamati ya LAAC imebaini kuendelea kuzorota kwa ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika baadhi ya Vyanzo vyake tegemezi vya makusanyo ambavyo vimeshikiliwa na Serikali kuu.

Mheshimiwa Spika, hadi ukaguzi huu unakamilika katika mwezi wa Novemba, 2022, Kampuni ya Serikali ya ZICTIA imeshidwa kutoa gawio linalotokana na makusanyo ya Minara kwenda kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa licha ya kuwa Kamati yako imewahi kulishauri hili katika ripoti zilizopita lakini bado changamoto hii imeshidwa kutatuka hadi leo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati ya LAAC inaendelea na kusikitishwa na kitendo cha baadhi ya Taasisi za Serikali Kuu zinazokusanya mapato kwa niaba ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kushindwa kuzipatia gawio la mapato yanayotokana na vianzio vyake.

Mheshimiwa Spika, muendelezo wa kitendo hicho kinachochea kwa kiasi kikubwa kupelekea Mamlaka za Serikali za Mitaa kushidwa kutekeleza majukumu yake ya usafi wa miji na kutoa huduma bora kwa wananchi kwa kuendeleza miradi mbalimbali ya kijamii kwa vile shughuli zote hizo zinahitaji fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, tutaendelea kuzilaumu Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa hazifanyi kazi zake ipasavyo wakati kiuhalisia Mamlaka hizo hazinufaiki na mapato yake yanayokusanywa kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inashauri Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kukaa pamoja na Taasisi zote zinazokusanya mapato kwa niaba ya Serikali za Mitaa ili kuzipatia ufumbuzi changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ripoti ya Mifumo ya TEHAMA imeendelea kubainika kuwepo kwa Mifumo ya TEHAMA katika Taasisi za Serikali ambayo haina tija na imekosa ufanisi katika utendaji kazi licha ya kuwa mifumo hiyo imetumia gharama kubwa katika ununuzi wake, hali hiyo inatokana na Taasisi hizo kukiuka taratibu mbalimbali za ununuzi wa Mifumo hiyo zikiwemo:

a) Kutoshirikishwa kwa Wakala wa Serikali Mtandao katika hatua za mwanzo hadi kukamilika kwa mfumo pindi Taasisi zinaponunua au kutengeneza Mifumo ya TEHAMA.

b) Kutofanyika kwa upembuzi yakinifu (feasibility study) pamoja na kuimarisha michakato ya biashara (business processes) juu ya mahitaji ya mifumo kwa Watumiaji kabla ya kuanzisha mifumo husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida Mdhibiti anapoibua hoja mbalimbali katika ripoti zake hutoa mapendekezo kwa ajili ya kutatua dosari hizo, cha kusikitisha ni kwamba mapendekezo yaliyotolewa katika Ripoti ya mwaka 2020/2021 katika Mifumo ya TEHAMA kwa kiasi kikubwa hayakufanyiwa kazi na Taasisi za Serikali kwa mfano,

TAASISI	DOSARI	UTEKELEZAJI
Ofisi ya Rais Fedha na Mipango	Taarifa za Hesabu za Hazina ambazo hazikuunganishwa na Mfumo wa IFMIS.	Haijatekelezwa
Wizara ya Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto	Kutotumika kwa mfumo wa ZUPS na MIS kufanya malipo ya kielektroniki	Haijatekelezwa

Mheshimiwa Spika, kitendo hicho kinarudisha nyuma utendaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwani Watendaji wa Afisi hii hutumia nguvu kubwa, rasilimali fedha na kadhalika katika kufanikisha shughuli hiyo muhimu kwa maendeleo ya nchi hii na matokeo yake tija iliyokusudiwa haipatikani.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kuyafanyia kazi maoni ya Mkaguzi Mkuu ili kupatikana mabadiliko chanja katika Taasisi zetu.

Mheshimiwa Spika, kiujumla Kamati ya LAAC imezipokea Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020 zinavyoelekeza na inaahidi kuzifanyia kazi Ripoti hizo kama Kanuni zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukurani tulizozitoa kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, tunaiomba Afisi hiyo wakati inatekeleza majukumu yake kuhakikisha kuwa inafuata misingi yote ya ukaguzi ili kuepusha malalamiko yasiyokuwa na lazima.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC wakati wa ufuatiliaji wa hoja za Mdhibiti katika Taasisi mbalimbali imebaini uwepo wa hoja ambazo kimsingi zilihitaji maelewano ya karibu tu baina ya Mkaguzi na Mkaguliwa kitu ambacho hukosekana na kupelekea uwepo wa hoja nyingi kwenye Taasisi moja.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inazitaka Taasisi za Serikali kutoa mashirikiano ya kutosha kwa Mkaguzi ikiwemo kutoa majibu yenye kujitosheleza ili kuepuka hoja zisizo na msingi.

Mheshimiwa Spika, mbali na hayo tunaiomba Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuendelea kuzipatia mafunzo Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zinazosimamia fedha ili Kamati hizi ziweze kuzifanyia kazi Ripoti hizi kwa uweledi mkubwa na kuweza kutoa maoni na mapendekezo yake bila ya kumpendelea au kumuonea mtu yeyote.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza hili, kwa utulivu wao na kwa kunisikiliza kwa makini wakati wote nilipokuwa nawasilisha maoni ya Kamati ya LAAC kuhusiana na Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa upande wa Mashirika, Taasisi Zinazojitegemea za Serikali, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Ripoti ya Mifumo ya TEHAMA kwa Taasisi za SMZ kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, pia, ninawaomba Wajumbe wako waitumie haki yao ya msingi iliyotolewa na kanuni ya 43(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi inayohusiana na kumuuliza maswali Mheshimiwa Waziri husika juu ya Ripoti hizi kwa lengo la kupata ufafanuzi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.



.....

Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma,
Makamo Mwenyekiti,
Kamati ya LAAC,
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar.